

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKO NA SERIKALI ZA MITAA**

Mkoa wa Dodoma
Anwani ya Simu REGCOM
Simu: 026 2324343/2324384
Nukushi: 0262320046/2320121
Barua pepe : ras@dodoma.go.tz



Ofisi ya Mkuu wa Mkoa
S.L.P. 914
Dodoma

TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

Serikali ya Mkoa wa Dodoma imeahidi kushirikiana na Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) na Jeshi la Magereza kwenye shughuli za kilimo kwa lengo la kuongeza uzalishaji wa chakula kitakachotosheleza mahitaji ya JKT na Magereza kwenye Kambi zao, mahitaji ya chakula kwenye Mkoa wa Dodoma na ziada kupelekwa Serikalini ili kusaidia maeneo Mengine yenye mahitaji.

Mkakati huo umetangazwa Leo Septemba 8, 2017 na Mkuu wa Mkoa wa Dodoma Mheshimiwa Jordan Rugimbana wakati wa sherehe za kuhitimisha mafunzo ya JKT kwa mujibu wa sheria **operesheni Tanzania ya viwanda** ambapo jumla ya vijana 964 wamehitimu mafunzo hayo kwenye kambi ya Jeshi (834 KJ) Makutupora nje kidogo ya Mji wa Dodoma.

Mheshimiwa Rugimbana amesema Mkakati huo wa kuondoa tatizo la upungufu wa chakula Mkoani Dodoma ni utekelezaji wa agizo la Rais Magufuli la kuhakikisha kila Mkoa unajitosheleza na kujitegemea kwa chakula ambapo ameahidi pamoja na maeneo ya kilimo yanayomilikiwa na Majeshi hayo, Mkoa utaona namna ya kuwaongezea maeneo mengine zaidi kwa ajili ya kilimo.

“Tayari wamejitokeza baadhi ya taasisi ambazo zimekubali kufadhili shughuli za kilimo Mkoani Dodoma na naahidi nitatoa kipaumbele kwa vyombo hivi ili visaidie kuimarisha shughuli za kilimo na uzalishaji wa chakula Mkoani Dodoma” Aliongeza Mheshimiwa Rugimbana.

Aliwataka vijana hao waliohitimu mafunzo ya JKT kuzingatia viapo vyao na kuwa raia wema na mabalozi wa Taifa letu kwa kujiepusha na kupinga vitendo vyote viovu ambapo ameahidi kuwa serikali ya Mkoa wa Dodoma itawapatia vijana hao kipaumbele kwenye kupata ajira mbalimbali kwenye mradi mkubwa wa bomba la mafuta kutoka nchini Uganda hadi Tanga ikizingatiwa kwa Mkoa wa Dodoma bomba hilo litapita kwenye Wilaya mbili (2) za Chemba na Kondoa.

Awali Kamanda Kikosi cha 834 KJ Luteni Kanali Aristide Rutta alibainisha kuwa vijana hao 964 waliohitimu wakiwa kambini hapo wamepatiwa mafunzo mbalimbali yakijumuisha nyanja za Uhodari, Medani, Ukakamavu, Uzalendo, Nidhamu, Uzalishaji kilimo na mafunzo ya darasani yanayojojumuisha mambo mengi.

Jeremia Mwakyoma

AFISA HABARI NA UHUSIANO - OFISI YA MKUU WA MKOA DODOMA
Septemba 8, 2017